102/3
KISWAHILI
KARATASI YA 3
(FASIHI)
JULAI/AGOSTI - 2014
MUDA: SAA 2 ½

For More Free KCSE Past papers Visit www.freekcsepastpapers.com

# TATHMINI YA SHULE ZA UPILI ZA JIMBO LA MERU - 2014

*Cheti cha Kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya.*

102/3
**KISWAHILI**
KARATASI YA 3
**(FASIHI)**
JULAI/AGOSTI - 2014
**MUDA: SAA 2 ½**

**MAAGIZO**

a) Jibu maswali manne **pekee**
b) Swali la **kwanza** ni la **lazima**
c) Maswali hayo mengine **matatu** yachaguliwe kutoka sehemu **nne** zilizobaki; yaani: Tamthilia, Ushairi, Hadithi Fupi na Fasihi simulizi.
d) Usijibu maswali **mawili** kutoka **sehemu moja**
e) Majibu yote **lazima** yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili

***Karatasi hii ina kurasa 4 zilizopigwa chapa.***
***Mtahiniwa wahakikishe kuwa kurasa zote nne za karatasi hii ya mtihani zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.***

## SEHEMU A: RIWAYA

**Ken Walibora: Kidagaa Kimemwozea**

1. **Lazima**

Riwaya ya kidagaa kimemwozea imeangazia uozo katika jamii. Jadili. (al. 20)

## SEHEMU B: TAMTHILIA

**T.Arege: Mstahiki Meya**

**Jibu swali la 2 au 3**

2. Tamthilia ya Mstahiki Meya ni kielelezo cha matatizo yanayozikumba nchi nyingi barani Afrika. Thibitisha. (al. 20)

3. "Sina pingamizi maana hii ni grand idea…"

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (al. 4)

(b) Bainisha tamathali moja ya usemi inayojitokeza katika dondoo hili. (al. 2)

(c) Eleza dhana ya grand idea. (al. 8)

(d) Fafanua sifa za msemaji. (al. 6)

For More Free KCSE Past papers Visit www.freekcsepastpapers.com

## SEHEMU C: USHAIRI

4. **Soma Shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.**

**TUJIBUNIE KAZI**

Nimeishi kushangaa, kwa wanaotafuta kazi,
Wanaobugia Chang'aa, mtaani wakibarizi,
Wanaoshinda kwa njaa, wakiamba hamna kazi
Kazi zina wenyeewe, jibunie yako kazi.

Jibunie kazi yako, utakayofurahia,
Kuwa randa ja mbwa koko, utabaki bila mia,
Ujifunze kula ukoko, huku ukijisevia,
Kazi zina wenyeewe, jibunie yako kazi.

Ujikaze kibaba, aushi kibadili,
Uepuuke uhaba, maisha uwe kamili,
Uishi ja Alibaba, ulimiliki mahoteli,
Kazi zina wenyeewe, jibunie yako kazi.

For More Free KCSE Past papers visit www.freekcsepastpapers.com

Tumia yako razini, ul'opewa na muweza,
Utakuja kubaini, kuwa wewe unaweza,
Ukipata upinzani, piganiya utaweza,
Kazi zina wenyeewe, jibunie yako kazi.

Wangapi tumewaona, wal'oanza mashinani,
Wakizibeba banana, kutoka kule kondeni,
Walizidi kupambana, wakamiliki kampuni,
Kazi zina wenyeewe, jibunie yako kazi.

Tamati miye nafika, jamvi langu nalikunja,
Nayosema ya hakika, ambayo nishayaonja,
Musije mukanitandika, kidhani miye mujanja,
Kazi zina wenyeewe, jibunie yako kazi.

**Maswali**

(a) Ni nini dhamira ya Mshairi. (alama 2)

(b) Eleza umuhimu wa kibwagizo. (alama 2)

(c) Fafanua kwa kutoa mfano, mbinu tatu alizotumia mshairi kutosheleza mahitaji ya kiarudh katika shairi. (alama 6)

(d) Taja tamathali yoyote moja inayojitokeza katika shairi. (alama 2)

(e) Andika ubeti wa nne kwa lugha ya nathari. (alama 4)

(f) Bainisha toni ya shairi hili (alama 2)

(g) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumiwa katika shairi. (alama 2)

 (i) Wakiamba

 (ii) Watabaki bila mia.

## SEHEMU E: HADITHI FUPI

**K. Walibora na S.A Mohamed : Damu Nyeusi na Hadithi nyingine.**

**Jibu swali la 5 au 6**

5. Eleza ufaafu wa anwani ya hadithi ya Shaka ya Mambo. (al. 2(

6. „Alijitumainisha kuwa kuna siku mume wake angetanabahika na yote yale yatafikia mwisho. S: yenyewe ni lini hasa?"

 (a) Eleza mambo ambayo mhusika alitumai yangefika mwisho. (al. 1

 (b) Taja tamathali yoyote <u>moja</u> inayojitokeza katika dondoo (al. 2

 (c) Eleza sifa za anayejitumainisha (al. 8

## SEHEMU D: FASIHI SIMULIZI

For More Free KCSE Past papers Visit www.freekcsepastpapers.com

**Jibu swali la 7 au 8**

7. (a) Maigizo ni nini ? (al. 2)
   (b) Eleza umuhimu wa maigizo. (al. 8)
   (c) Toa mifano miwili ya miviga. (al. 2)
   (d) Eleza sifa nne za Miviga. (al. 8)

8. (a) Taja aina za ngomezi. (al. 2)
   (b) Eleza udhaifu wa ngomezi. (al. 8)
   (c) Eleza maandalizi yanayopaswa kufanywa na mtafiti wa fasihi simulizi. (al. 10)